TANGAZO LA SERIKALI NA. 315 la tarehe 25/08/2017

(SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA, (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 89*

SHERIA NDOGO ZA (MATUMIZI YA BARABARA) ZA HALMASHAURI YA MJI NZEGA ZA MWAKA 2017

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Matumizi ya Barabara) za Halmashauri ya Mji Nzega za Mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Mji Nzega.

Tafsiri.

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Halmashauri"maana yake ni Halmashauri ya Mji Nzega;

"Kituo cha basi" maana yake ni kituo kilichotengwa mahsusi kwa ajili ya kuegesha mabasi yanayoshusha na kupakia abiria;

"Kituo cha teksi" maana yake ni kituo kilichosajiliwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha teksi;

"Lori" maana yake ni gari yoyote ile ya kubeba mzigo yenye uzito kuanzia tani tatu na nusu na kuendelea;

"Chombo cha moto" maana yake ni gari, bajaji, pikipiki na chombo kingine chochote cha moto chenye kutumia magurudumu kinachotumia nishati ya Petroli, Dizeli au gesi au umeme;

“ Maegesho” maana yake ni sehemu yeyote iliyotengwa mahsusi na Halmashauri kwa ajii ya kuegesha vyombo ya moto;

“Mkokoteni: maana yake chombo chochote kile chenye magurudumu kinachotumika kubeba mizigo ambacho hutembea kwa kusukumwa na binandamu au kukokokotwa na mnyama, itajumuisha guta;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Nzega;

“Afisa mwidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

“Mtaa” maana yake eneo lolote ndani ya Halmashauri ya Mji Nzega na inajumuisha barabara;

“Teksi” maana yake ni gari yoyote iliyosajiriwa yenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi wanne inayotumika kufanya biashara ya kusafirisha watu;

“Wakala” maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo litakuwa limepewa mamlaka na Halmashauri ya kutekeleza Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Halmashauri.

Maegesho

4. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha chombo cha moto au mkokoteni nje ya eneo lililotengwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri kwa kushirikiana na vyombo vingine itaweka alama za barabarani za kuonyesha sehemu iliyotengwa kwa ajili ya kuegesha vyombo vya moto au mkokoteni katika maeneo yote ndani ya Halmashauri.

Usajili wa teksi

5. (1) Kila teksi itatakiwa kusajiliwa na Halmashauri kabla ya kuanza kufanya biashara ya kusafirisha abiria.

(2) Mmiliki wa teksi atahakikisha kwamba gari lake limekaguliwa na limelipiwa kodi zote zinazotakiwa na Serikali ikiwa ni pamoja na ada za Halmashauri.

(3) Ni wajibu wa kila mmiliki wa teksi kuchora mstari wa kijani ubavuni mwa teksi, kuweka taa juu ya teksi yake (Noon lamp) na anuani kabla ya teksi kukaguliwa na kusajiliwa.

(4) Baada ya teksi kusajiliwa, Halmashauri itatoa namba na ubavuni na kuainisha kituo ambacho teski iliyosajiliwa itaegeshwa.

(5) Kila usajili wa teksi utadumu kwa muda wa mwaka mmoja, baada ya hapo mmiliki wa teksi atawajibika kurudia usajili wa teksi yake mwaka ni kipindi kati ya Julai hadi Juni.

(6) Teksi iliyosajiliwa endapo haitakuwepo kituoni kwa kipindi cha miezi mitatu mfululizo itafutiwa usajili.

(7) Ni marufuku kwa gari lolote lisilosajiliwa kufanya biashara ya teksi (Teksi Bubu).

Usajili wa vituo vya teksi

6 . (1) Halmashauri itatenga na kusajili maeneo rasmi kwa ajili ya kutumika kama vituo vya teksi.

(2) Halmashauri itabainisha idadi ya teksi zitakazoruhusiwa kuegeshwa katika kituo kimoja kwa wakati mmoja kwa kuzingatia ukubwa wa eneo husika.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha teksi mahali ambapo hapajatengwa rasmi kwa matumizi hayo.

Mikokoteni

7 . (1) Ni wajibu wa kila mwenye mkokoteni kuusajili mkokoteni wake kwenye Kata anayoegesha mkokoteni.

(2) Afisa Mtendaji wa Kata husika ataupatia namba mkokoteni huo na kuupangia eneo ambalo utatakiwa kuegeshwa ndani ya Kata husika.

(3) Kila mkokoteni utalipiwa ada ya usajili kama itakavyopangwa na Halmashauri.

Barabara na uzito wa magari

8. (1) Kila barabara itakua na alama inayoonesha uzito wa magari yanayoruhusiwa kupita katika barabara hiyo. Halmashauri itaweka katika kila barabara bango linaloonyesha uzito wa magari yanayoruhusiwa kupitishwa katika barabara hiyo.

(2) Hakuna lori na/au gari lolote litakalo ruhusiwa kupitishwa katika barabara yoyote iwapo uzito wa gari hilo utakuwa mkubwa kuliko uzito wa magari yaliyoruhusiwa kupitishwa katika barabara hiyo.

Malori

9. (1) Ni marufuku kwa lori au kontena lolote kuingia eneo lote la Halmashauri bila ya kupata idhini ya maandishi ya Halmashauri.

(2) Kibali kilichotolewa kitatumika kwa safari moja kwa siku moja kwa muda uliotajwa kwenye kibali na kwa barabara zitakazoainishwa ndani ya kibali hicho.

(3) Kibali cha kuingiza malori au makontena kitatolewa na Mkurugenzi baada ya kupokea maombi ya maandishi kutoka kwa mwombaji yakiainisha lengo la kuingiza lori au kontena katika eneo la Halmashauri muda na mahali lori hilo linapokwenda.

Uoshaji wa magari

10. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuosha chombo cha moto eneo la barabara, hifadhi ya barabara au eneo la wazi ambalo halikutengwa kwa matumizi ya kuosha magari.

(2) Mmiliki wa gari iliyovutwa kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi atatakiwa kulipa faini iliyohainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi na gharama za kuvuta gari pamoja na gharama ya kutunza gari hilo iwapo litatunzwa kwenye eneo la Halmashauri au kiwango cha gharama kitakachobainishwa na mmiliki wa eneo la kuhifadhi gari.

(3) Mtu yeyote atakayekutwa anaosha chombo cha moto eneo lisiloruhusiwa atakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya Sheria.

(4) Iwapo chombo cha moto kilichovutwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kitakaa katika ofisi za Halmashauri kwa muda wa siku kumi na nne bila ya kuchukuliwa na mmiliki wake, Halmashauri itakiuza chombo hicho kwa mnada baada ya kupata kibali kutoka mahakamani ili kufidia gharama zake na kiasi cha fedha kitakachobaki atarudishiwa mmiliki wa chombo.

Ufungaji wa barabara

11. Ni marufuku kwa mtu yeyote kufunga barabara kwa ajili ya sherehe, msiba au shughuli nyingine yoyote ile bila kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi.

Uwekaji wa vifaa vya ujenzi barabarani

12. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka au kumwaga vifaa vya ujenzi kama kokoto, mchanga, kifusi, mawe na vifaa vinginevyo vya ujenzi kwenye barabara, hifadhi ya barabara au eneo lisiloruhusiwa bila ya idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

Kukata barabara

13. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata barabara kwa ajili ya kupitisha mabomba ya maji, nyaya za umeme, simu au shughuli nyingine yoyote ile bila ya kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi na kulipia ada ya kukata barabara kama inavyooneshwa katika Jedwali la kwanza katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Kibali cha kukata barabara kitadumu kwa muda wa siku saba na baada ya hapo endapo muombaji atashindwa kurekebisha eneo lililokatwa na

kurejesha barabara katika hali ya awali atachukuliwa hatua za kisheria.

Makosa na Adhabu

14. (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo:-

(a) Ataegesha chombo cha moto katika sehemu isiyoruhusiwa;

(b) Atafanya biashara ya teksi kwa kutumia gari ambayo haijasajiliwa au ataegesha teksi kwenye eneo ambalo sio kituo cha teksi;

(c) Ataendesha mkokoteni ambao haujasajiliwa;

(d) Ataendesha mkokoteni katika barabara ambayo haijaruhusiwa;

(e) Ataingiza lori au kontena katika eneo la Halmashauri bila kibali;

(f) Ataosha chombo cha moto katika eneo la barabara, hifadhi ya barabara au eneo la wazi ambalo matumizi yake siyo ya kuoshea magari;

(g) Atafunga barabara kwa shughuli za sherehe, msiba au shughuli nyingine yoyote bila kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi;

(h) Atakata barabara bila kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi;

(i) Ataweka au kumwaga vifaa vya ujenzi kwenye barabara, hifadhi ya barabara au eneo lisiloruhisiwa;

(j) Atamzuia Afisa au Wakala wa Halmashauri kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ndogo hizi;

(2) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=), au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Uwezo wa Kufifilisha Kosa.

15. Mkurugenzi anaweza kumtoza faini isiyozidi shilingi elfu thelathini (30,000/=) mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mkosaji atakiri kosa hilo kwa hiari yake mwenyewe na kujaza fomu maalumu na atapewa stakabadhi mara baada ya kulipa faini.

———

JEDWALI

———

*Limetungwa chini ya kifungu cha 13(1)*

ADA YA KUKATA BARABARA

(i) Tsh.200,000/=....................... kwa kila mita kwa barabara ya lami

(ii) Tsh. 15,000/=....................kwa kila mita kwa barabara ya vumbi

JEDWALI LA PILI

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 15)*

Mimi …………………………… wa S.L.P. ………., ………………………………. Nimekiri kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nimetenda kosa la ………………………… katika Eneo la Halmashauri ya Mji Nzega kosa ambalo ni kinyume na na kifungu cha ……………… cha Sheria ya Ndogo za ( Matumizi ya Barabara) za Halmashauri ya Mji wa Nzega za Mwaka 2017.

Kwa hiyo, Kwa hiari yangu mwenyewe pasipo kushawishiwa na mtu yeyote nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya Kifungu cha 15 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini:………………………………………………...

Mbele yangu:-
Jina:…………………………………………….
Saini:……………………………………………
Wadhifa: ………………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa Nzega limebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 25 mwezi 10 Mwaka 2016.

PHILEMON M. MAGESA,
*Mkurugenzi wa Mji,*
*Halmashauri ya Mji wa Nzega*

WILLIAM W. JOMANGA,
*Mwenyekit wa Halmashauri,*
*Halmashauri ya Mji wa Nzega*

NAKUBALI

Dodoma,
13 Julai, 2017

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB.),
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI*